

**SALAMUA ZA MKUU WA MKOA WA RUKWA MHE.
MAGALULA SAID MAGALULA ALIZOZITOA WAKATI WA
KILELE CHA WIKI YA SHERIA NCHINI KANDA YA
SUMBAWANGA TAREHE 04 FEBRUARI, 2016**

Mheshimiwa Jaji Mfawidhi, Kanda ya Sumbawanga,

Mheshimiwa Jaji Kassim M. Nyangarika, Jaji wa Mahakama Kuu
Kanda ya Sumbawanga.

Wakili wa Serikali Mfawidhi wa Mkoa wa Rukwa,

Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga,

Waheshimiwa Viongozi wa Madhehebu ya Dini,

Mheshimiwa Msajili wa Wilaya, Kanda ya Sumbawanga

Waheshimiwa Mawakili wa Serikali na Wakujitegemea,

Waheshimiwa Mahakimu,

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya
ya Sumbawanga.

Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa,

Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Viongozi wa Taasisi za Umma na Taasisi binafsi,

Watumishi wa Mahakama,

Ndugu Waandishi wa Habari,

Wageni waalikwa,

Mabibi na Mabwana.

Napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kushiriki kilele cha maadhimisho ya wiki ya sheria Nchini.

Kama inavyofahamika Nchi yetu inaongozwa na mihimili mitatu “Mahakama, Bunge na Utawala”

Binafsi nimefarijika namna ambavyo mihimili hii inavyoshirikiana. Nchi yetu inaongozwa kwa misingi ya Utawala wa Sheria. Hivyo ili nchi hii iweze kutawalika tunapata miongozo katika Mhimili wa Mahakama ambako ndiko mliko bobobea katika kutafsiri sheria za Nchi yetu.

Hivyo basi katika neno langu hili la salaamu, napenda kutoa wito kwetu sote tuenzi ushirikiano huu uliopo ili tuweze kuwatendea “Haki” Wananchi wetu.

Natoa Wito kwetu sote Wadau tuliopo hapa, kwa kuwa sote nia yetu ni moja kuhakikisha Mwananchi anapata “Haki” katika mfumo wa mahusiano ya Serikali na Taasisi nyingine ikiwemo Taasisi za Umma, binafsi na Taasisi za dini. Hivyo tuzidishe umoja miongoni mwetu. Umoja ambao peke yake utapelekea baadhi ya changamoto kupungua katika suala zima la kumpatia mwananchi “Haki”

Baada ya Maadhimisho haya ni mwanzo wa shughuli za Mahakama kwa Mwaka 2016. Napenda kuwatakieni kila la heri katika majukumu yenu ya kuhakikisha mnasimamia “Haki” Mwenyezi

Mungu awatangulie katika jukumu hilo zito “Jukumu hilo ni zito kwa kuwa mmebeba dhamana ya kusimamia na kuhakikisha “Haki” inatendeka. Kama ambavyo inafahamika kupitia Maandiko matakatifu Jukumu hilo pia lilitokelezwa na Mitume na Manabii wa Mungu kwa niaba ya Mungu.

Kutekeleza Jukumu hilo inahitajika uadilifu wa hali ya juu.

Mimi binafsi nawenzangu nitatoa ushirikiano bila kusita ili kuhakikisha “Haki” za Wananchi wetu zinatolewa bila kikwazo chochote sawa sawa na kauli mbiu yetu ya leo **“HUDUMA ZA HAKI KUMLENGA MWANANCHI: WAJIBU WA MAHAKAMA NA WADAU”** tutatekeleza wajibu wetu kama Wadau wa Mahakama.

Napenda kuhitimisha kwa kushukuru Wadau wote ndani ya Mkoa kwa ushirikiano mnaotupatia katika kuleta maendeleo ndani ya Mkoa, tuzidi kushirikiana kila mmoja anahitaji mchango wa mwingine, na kila mmoja miongoni mwetu ni muhimu katika maendeleo ya Mkoa

Asanteni kwa kunisikiliza.

Magalula S. Magalula
MKUU WA MKOA RUKWA